AFRIKA



KANISA LA MNAZARETI - AFRIKA

# SIKU 21 YA MAOMBI 2026

## BWANA UTUFUNDISHE KUOMBA IPASAVYO

Waefeso 3:10

# Siku 21 za Maombi 2026

## Utangulizi: “Bwana, Tufundishe Kuomba”

## Waefeso

Wanafunzi walikuwa wametembea na Yesu. Walikuwa wameona miujiza, kusikia mafundisho Yake, na kushuhudia uponyaji Wake. Lakini kilichowagusa zaidi haikuwa tu matendo hayo, bali ni ule ukaribu na ushirika wa kiungu aliokuwa nao na Baba. Ilikuwa ni ile hali ya ukaribu wa kina na Baba yake iliyowasukuma kuuliza, **“Bwana, tufundishe kuomba.”**

Katika roho hiyo hiyo, tunamjia Yesu leo tukiwa na shauku hiyo hiyo. Kama Kanisa la Nazarene katika bara la Afrika, tunaingia katika kipindi cha siku 21 za maombi. Hatujadhamiria kutafuta mbinu au kanuni; tunatafuta ukaribu. Tunasema: **“Bwana, nifundishe kuomba. Tufundishe kuomba.”**

Kwa kuliongoza kipindi hiki, tumechagua kitabu cha Waefeso. Ingawa Paulo anashughulikia mada nyingi, Waefeso hatimaye ni kitabu cha mwaliko wa kiroho wa kina. Kinatuvuta katika ukaribu na Yesu, na Baba, na fumbo la Mungu wa Utatu. Kinatuwekea mizizi katika utambulisho wetu ndani ya Kristo ili maombi yetu yatiririke kutoka kwenye mamlaka ya kiroho na undani wa mahusiano yetu naye.

Andiko letu kuu ni **Waefeso 3:10:**

*“Ili sasa kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na enzi na mamlaka katika ulimwengu wa roho.”*

Ayahii ndiyo inayobeba moyo wa maombi yetu. Tunaomba kwamba hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi idhihirishwe kupitia sisi, ndani yetu, na kwa ulimwengu wa roho. Tunaomba si tu majibu, bali mwafaka na makusudi ya milele ya Mungu.

## Hivyo tunakukaribisha kujiunga nasi kwa mpangilio wa kila wiki:

**Wiki ya 1 – “Bwana, nifundishe kuomba”:** kama mtu binafsi, ukitafakari juu ya utambulisho wako ndani ya Kristo.
**Wiki ya 2 – “Bwana, tufundishe kuomba”:** kama familia, tukiinua kila mmoja katika upendo na umoja.
**Wiki ya 3 – “Bwana, tufundishe kuomba”:** kama Kanisa, tukiombea jamii zetu, bara letu, na mwili wa Kristo wa duniani kote.

Tunakupongeza usisome tu vifungu maalumu vilivyopangwa, bali kitabu chote cha Waefeso unapomtafuta Mungu kwa bidii. Na iwe ni wakati wa kukutana kwa undani na Mungu. Mungu na atende kazi kupitia na ndani yetu tunapoomba. Na nasi, kama wanafunzi, tubadilishwe na ule ukaribu tunaougundua.

Baraka tele unapoanza safari hii ya kipekee.

# Jedwali la Yaliyomo

**WIKI YA 1**
Siku ya 1: Hakikisho La Baraka 2
Siku ya 2: Hekima ya kiroho na tumaini la ujasiri 3
Siku ya 3: Nguvu zilizomfufua Yesu 4
Siku ya 4: Utambulisho katika Kristo 5
Siku ya 5: Enendeni kwa thamani ya wito wenu 6
Siku ya 6: Kuyaweka kando ya kale na kuvaa mapya 7
Siku ya 7: Wanaoiga Mungu 8

**WIKI YA 2**
Siku ya 8: Baraka za Mungu zinazomiminika juu yetu 9
Siku ya 9: Nyumba ya neema 10
Siku ya 10: Maombi ya wanandoa na mahusiano 11
Siku ya 11: Maombi ya wazazi na watoto (mahusiano) 12
Siku ya 12: Wafanya amani 13
Siku ya 13: Mahusiano kazini 14
Siku ya 14: Vita vya kiroho katika familia 15

**WIKI YA 3**
Siku ya 15: Kusudi la Mungu kwa Kanisa 16
Siku ya 16: Umoja na Kristo 17
Siku ya 17: Rasilimali Isiyo na kikomo 18
Siku ya 18: Kuandaliwa kwa ajili ya huduma 19
Siku ya 19: Kukua pamoja katika upendo 20
Siku ya 20: Kito cha Mungu 21
Siku ya 21: Vita vya kiroho kanisani 22



# Siku ya 1: Hakikisho La Baraka

## Waefeso 3:13-14

*Ukishaamini, uliwekewa alama ndani yake kwa muhuri, Roho Mtakatifu aliyeahidiwa, ambaye ni amama anayetuhakukushia urithi wetu hadi ukombozi wa wale walio mali yake-kwa sifa ya utukufu wake.*

### Ibada:


Tunapoanza kuamini, Mungu hutupa Roho Mtakatifu kama hakikisho la kuonyesha kuwa tumeasiliwa kwa familia ya Mungu. Ni Roho Mtakatifu ndiye Anatusaidia kumfikia Mungu kama Baba wetu. Kama mtoto yeyote anayemwendea mzazi ili akumbatiwe, na upendo, akiwa na hitaji, furaha, huzuni, kuumia au hitaji tu la ukaribu na mzazi wako. Hivyo ndivyo yalivyo maombi, kumkaribia Baba wet una kuwa katika uweponi mwake. Japo dhambi ilitutenganisha, ndani ya Kristo na kupitia kwa Kristo tunapatanishwa ndani ya Familia ya Mungu tunapoamini, tunapokea urithi. Kuwa warithi inamaana kuwa tunazo raslimali za kiroho na baraka kwaajili yetu. Tunaweza kuwa na ukaribu, ushirika na umoja pamoja na baba wetu wa Mbinguni na tunaweza kutumia raslimali zilizotolewa kwaajili yetu. Roho Mtakatifu anatuhakikishia ukweli hu una kututia nguvu ili tuishi kama Watoto wa Mungu.

### Tafakari:

Je unalo hakikisho hili la baraka kuwa wewe ni mrithi-mwenza na Kristo, hakikisho ambalo linakupa ujasiri kuwepo uweponi mwa Mungu kwaajili ya lolote na yote kama mtoto ananyokuwa katika uwepo wa mzani wake?

### Ombi:

Baba wetu wa Mbinguni, umetupa Roho wako, Roho Mtakatifu, ili atukumbushe sisi ni nani ndani ya Kristo. Naomba nihisi hakikisho kuwa wewe ni mzazi wangu, na ninaweza kuwa uweponi mwako wakati wowote pasipo na shaka, uwoga au hatia. Amina.



# Siku ya 2: Hekima ya kiroho na tumaini la ujasiri

**Waefeso 1:15, 17-18**

*15 Kwa sababu hii, tangu niliposikia juu ya imani yenu katika Bwana Yesu na upendo wenu kwa watu wote wa Mungu,*
*17 siachi kumwomba Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba mtukufu, awape Roho wa hekima na ufunuo ili mpate*
*kumjua zaidi. 18 Ninasali ili macho ya mioyo yenu yatiwe nuru mpate kujua tumaini ambalo amewaitia, na utajiri wa*
*urithi wake mtukufu katika watu wake watakatifu.*

### Ibada:

Maombi huonyesha yaliyomo katika mioyo na mawazo yetu. Hufichua matamanio yetu, tamaa na matarajio yetu. Wakati mwingine tunapoomba hadharani, tunachuja mawazo yetu na kuchagua maneno yetu ili tusikike vizuri machoni pa wengine. Wakati mwingine mtazamo huo huo hutokea hata tunapoomba faraghani. Mtazamo huu hutunyima maombi ya kweli na uhusiano wa dhati na Mungu. Lakini tunaye sababu ya kufurahi kwa kuwa Baba anatupenda kiasi cha kutupa Roho wake. Roho wa hekima na ufunuo ni zawadi kutoka kwa Mungu na ni ishara ya ukuaji wa kiroho. Tunapokuwa na Roho huyu, tunamtumikia Mungu vizuri zaidi na kwa uhalisia. Naye ataangaza macho ya mioyo yetu na kuimarisha imani yetu kwa Mungu, ambayo kupitia hiyo tutamjua Mungu ni nani, sisi ni nani ndani ya Kristo na tumaini alilotuitia, na tutaweza kufurahia utajiri wa utukufu wake. Hekima ya kiroho hutuwezesha kuwa watu wa kweli mbele za Mungu. Hufichua mioyo yetu, tamaa zilizofichika na matumaini ya uongo ambayo huenda tumekuwa tukijiegemeza juu yake. Moyo wetu na ufunuliwe ili tukue katika imani na kutembea na Kristo.

### Tafakari:

Je, Roho wa hekima na ufunuo anakusaidia kumtumikia Mungu kwa njia bora zaidi, na kukusaidia kujua tumaini ambalo umeitiwa?

### Ombi:

Bwana mpendwa, nakushukuru kwa imani yangu kwako leo, naomba ufunue macho ya moyo wangu nipate kujua tumaini ulilonitia. Naomba unipe Roho wa hekima na ufunuo ili nikutumikie kwa njia iliyo bora zaidi. Amina.



# Siku ya 3: Nguvu zilizomfufua Yesu

**Waefeso 1:19-23**

*Na uweza wake mkuu usiopimika kwa ajili yetu tuaminio. Uweza huo ni sawa na ile nguvu yake kuu aliyotumia alipomfufua Kristo kutoka kwa wafu.*

**Ibada:**
Paulo anatuambia kwamba ile ile nguvu iliyomfufua Kristo kutoka kwa wafu sasa ika ndani yetu. Si nguvu iliyo punguzwa, wala si toleo dhaifu, bali ni nguvu ile ile. Neno la Kigiriki linalotumika hapa kwa "nguvu" ni dynamis—chanzo cha neno letu "dynamite." Ni nguvu inayolipuka, isiyoweza kuzuiliwa, na ya kimungu. Ilivunja nguvu za mauti, ikamtukuza Yesu juu ya mamlaka yote, na ikamketisha mkono wa kuume wa Mungu. Na sasa nguvu hiyo inafanya kazi ndani yetu.

Tunapoomba, tunapoishi, au tunapohudumu, hatupaswi kutegemea nguvu za kibinadamu kama wale wasiouamini. Tunaweza kuunganishwa na nguvu za ufufuo. Hatuko hapa tu kupambana na vita vya kiroho, bali tunashiriki ushindi wa Kristo. Nguvu hii hutuwezesha kunena uzima katika maeneo yaliyovunjika, kuturejesha upya na kubadilisha jamii zetu.

**Tafakari:**
Tafakari eneo la maisha yako ambako unahisi huna nguvu. Mkaribishe Roho Mtakatifu akufunulie jinsi nguvu za ufufuo zinavyotaka kutenda kazi katika eneo hilo.

**Ombi:**
Bwana, nifufue katika ufahamu wa nguvu zilizomfufua Yesu kutoka kwa wafu. Nisaidie kuishi, kupenda, na kuhudumu kutoka kwenye mamlaka ya ufufuo. Maisha yangu yaakisi ushindi wa kaburi tupu na utawala wa Kristo juu ya vitu vyote. Amina.



# Siku ya 4: Utambulisho katika Kristo

**Waefeso 2:4-6**

*Lakini kwa sababu ya upendo wake mkuu alio nao kwa ajili yetu, Mungu aliye mwingi wa rehema, alituhuisha pamoja na Kristo hata tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu—mmeokolewa kwa neema. Naye Mungu akatufufua pamoja na Kristo na kutukalisha pamoja naye katika ulimwengu wa mbinguni ndani ya Kristo Yesu.*

## Ibada:

Kujua wewe ni nani ni muhimu kwa maisha ya maombi yenye afya. Usipofahamu utambulisho wako, hofu na mashaka vitakuzuia kumkaribia Mungu. Lakini unapojifahamu, hata pamoja na mapungufu yako na makosa yako, unaweza kumwendea Mungu na kukiri kwamba unahitaji neema yake kila siku. Ndiyo, sisi ni wenye dhambi. Ndiyo, tunakosea. Ndiyo, tunatenda mabaya. Na ndiyo, Kristo alikufa kwa ajili yetu. Ndiyo, alifufuliwa kwa ajili yetu. Na ndiyo, Mungu anatuhisha pamoja na Kristo. Kujielewa sisi wenyewe pamoja na mitazamo yetu, fikra zetu na tamaduni zetu ni vizuri zaidi tukifanya hivyo katika nuru ya Injili. Hapo ndipo tunaweza kuomba bila aibu wala kiburi. Hapo tunaweza kuomba tukijua na kukubali nafasi yetu katika Ufalme wa Mungu.

## Tafakari:

- Ni utambulisho gani umekuwa ukiunda maombi yako?
- Je, utambulisho wako katika Kristo unaathiri jinsi unavyoomba?

## Ombi:

Baba wa Mbinguni, tunakusifu kwa kuwa hukutuacha tukiwa wafu katika makosa yetu. Tusaidie tujione kwa usahihi—si kama watu wasio na thamani, wala si kama wakamilifu—bali kama unavyotuona. Tusaidie tuwe vile ulivyotuumba tuwe katika maisha yetu ya kila siku. Kwa jina la Yesu. Amina.



# Siku ya 5: Enendeni kwa thamani ya wito wenu

**Waefeso 4:1-3**

*Basi, mimi niliye mfungwa kwa ajili ya Bwana, nawasihi mishi maisha yanayostahili wito mlioitiwa. Iweni wanyenyekevu kabisa na wapole; mvumiliane, mkivumiliana ninyi kwa ninyi katika upendo. Jitahidini kudumisha umoja wa Roho kwa kifungo cha amani.*

### Ibada:

Licha ya mateso na dhiki zake kama mfungwa, Paulo anawahimiza waamini kudumisha maisha matakatifu kwa kuonyesha unyenyekevu, upole na uvumilivu. Zaidi ya hayo, utakatifu unapaswa kudhihirishwa katika upendo kwa Mungu na upendo kwa watu wengine. Kama Wakristo, tunatarajiwa kuishi maisha yanayostahili wito wetu. Tunaposhindwa kuishi maisha ya upendo na utakatifu, inakuwa vigumu kwetu kuomba, "utusamehe dhambi zetu kama tunavyowasamehe waliotukosea."

### Tafakari:

Ni kwa njia gani unaweza kuonyesha unyenyekevu, upole na uvumilivu katika mahusiano yetu ya kila siku?

### Ombi:

Bwana wetu Yesu Kristo, kwa kupitia Roho Mtakatifu, nisaidie kuishi maisha yanayostahili wito wetu. Kila siku tunaomba uongoze hatua zetu. Kwa unyenyekevu tunaomba Roho wako Mtakatifu atembelee nasi daima katika maisha yetu ya kila siku. Tnatamani kuishi maisha yanayokupendeza. Kwa jina la Yesu, Amina.



# Siku ya 6: Kuyaweka kando ya kale na Kuvaa mapya

**Waefeso 4:22-24**

*Mlifundishwa kwamba, kwa kuzingatia maisha yenu ya kale, mvue utu wenu wa zamani, ambao unaharibika kwa tamaa zake za udanganyifu; mfanywe upya katika roho ya nia zenu; na kuvaa utu mpya, ulioumbwa kufanana na Mungu katika haki ya kweli na utakatifu.*

**Ibada:**
Maisha ya dhambi yanasimama kinyume na Mungu na hayawezi kumpendeza. Njia pekee ya kumkaribia Mungu ni kupitia toba ya kweli. Hii ni kugeuka kabisa kutoka kwa asili yetu ya dhambi kwa unyenyekevu tukitafuta msamaha wa Mungu. Mabadiliko haya kwa msingi wake ni upyaisho wa nia. Leo, ujumbe wa toba umepungua sana katika mimbari zetu nyingi. Badala yake, mafundisho yanayolenga mabadiliko ya kimwili na mali yamepata nafasi kubwa katika makanisa yetu. Hata hivyo, Paulo anatukumbusha kwamba mabadiliko ya kiroho lazima yawe kipaumbele. Hatuwezi kupata uamsho wa kweli wa Kikristo barani Afrika ikiwa akili za waamini hazijafanywa upya na kubadilishwa kufanana na Kristo.

Kwa hiyo lazima tuendelee kuwaombea sio waamini wenzetu tu bali kanisa lote la Afrika na hata nje ya mipaka yake. Neno la Mungu linatufundisha kukataa tamaa zetu za udanganyifu na kutafuta haki ya Mungu, ambayo ndiyo sura mpya tuliyo nayo ndani ya Kristo Yesu. Kufanywa upya katika mfano wa Kristo ndicho kiashiria cha haki na utakatifu wa Mungu uliorejeshwa ndani yetu.

**Tafakari:**
Unapojichunguza kwa uaminifu, ni maeneo gani maalum ya moyo na mawazo yako bado yanahitaji kukabidhiwa kwa Mungu au kuwekwa kando kwa ajili ya mabadiliko?

**Ombi:**
Baba yetu wa Mbinguni, leo tunatafuta msamaha wako kwa unyenyekevu. Tunakuja mbele ya madhabahu yako tukiwa na mioyo ya heshima, tukijitoa kwako kama dhabihu hai, takatifu na inayokupendeza. Tumechagua kuyaacha maisha yetu ya kale, yaliyoharibika na yenye tamaa za udanganyifu ambazo daima zinapingana na mapenzi yako. Tusaidie tufe kwa asili yetu ya dhambi tunapovaa sura mpya iliyobadilishwa ya Kristo. Roho Mtakatifu, tunakukaribisha kutufanya upya katika nia na kurejesha haki na utakatifu wa Mungu ndani ya maisha yetu. Utubadilishe kutoka ndani hadi nje ili tuakisi utukufu wako na kutembea katika njia zako. Utufanye vyombo vya uamsho katika jamii zetu na kote Afrika, kuanzia na mioyo yetu iliyosalimishwa kwako. Kwa jina adhimu la Yesu tunaomba. Amina.



# Siku ya 7: Wanaoiga Mungu

**Waefeso 5:1**

*Nyinyi ni Watoto wapendwa wa Mungu, hivyo basi iweni alivyo. Maisha yenu yatawaliwe na upendo, kama Kriato Alivyotupenda na kutoa uhai wake kama sadaka yenye harufu nzuri na dhabihu nzuri kwa Mungu.*

**Ibada:**
Neno la Mungu linatualika kuwa kama Mungu. Na muhimu ni mfano wa jinsi anahisi kuhusu uumbaji wake, hadi kumtoa Mwanawe kufa kwaajili yetu msalabani, japo anafahamu kuwa sisi hatustahili, kwasababu ya makossa na upungufu wetu wa utukufu wa Mungu.

Kumuiga Mungu sio kuulazimisha ukamilifu lakini ni safari ya upendo. Yesu alikuwa mfano hai kwa kujitoa kwaajili yetu, kama sadaka yenye harufu nzuri. Tunapoongoza, kutumika na kuzungumzakutokana na upendo huo, Maisha yetu yanakuwa manukato ya neema katika familia zetu, Makanisa na Jamii. Kumuiga Mungu inamaanisha kupenda pasipo uwezekano, kusamehe pasipostahili kuongoza kwa unyenyekevu na sio majivuno. Huu ndio mfano wa upendo ambao unabadilisha, kuwezesha na kujenga.

**Tafakari:**
Je upendo kwa ndugu yako au dada yako ambao ni sehemu ya uumbaji ambao Mungu anapenda ni wa aina gani?

**Ombi:**
Baba Mtakatifi, muumba wa Ulimwengu, tunakuja kwako tukikuuliza utujaze na upendo kwaajili ya ndugu zetu na dada zetu walio duniani. Tupende Alivyotupenda Kristo, ili tuwe kama alivyo zaidi. Amina



# Siku ya 8: Baraka za Mungu zinazomiminika juu yetu

**Waefeso 1:3-8**

*Ahimidiwe Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki katika ulimwengu wa roho kwa kila baraka ya kiroho ndani ya Kristo. Kwa maana alituchagua ndani yake kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu ili tuwe watakatifu na wasio na lawama mbele zake.*

## Ibada:

Paulo anatuarika katika maisha ya sifa na ibada kwa Mungu wetu, Muumba wa mbingu na dunia. Anaonyesha wazi kwamba kabla dunia haijaanza, kabla ya nyota ya kwanza kung'aa, Mungu tayari alikuwa akiwaza kuhusu mwanadamu. Muumba wa ulimwengu aliweka upendo wake juu yetu na kutuchagua tuwe mali yake. Ni dhahiri, basi, kwamba haikuwa uamuzi wa haraka au wa dharura baada ya dhambi kuingia ulimwenguni. Ilikuwa ni chaguo lake la makusudi, lililojaa furaha na lililotokana na upendo mkamilifu. Ilikuwa "sawasawa na radhi yake na mapenzi yake." Mungu hakutuchukua kwa kusita au kwa kulazimika. Alifurahia kutufanya kuwa watoto wake.

Kupitia kazi ya ukombozi ya Kristo, tumepokea msamaha kwa neema yake. Ni muhimu kwa waamini kutambua kwamba ukweli huu unapaswa kubadilisha namna tunavyojiona sisi wenyewe na tunavyowaona wengine. Sisi si ajali zinazozunguka bila mwelekeo tukitafuta maana ya maisha. Sisi ni waliochaguliwa, waliokusudiwa kwa utukufu, waliokombolewa kwa damu, na waliomiminiwa kibali cha kimungu. Huu ndio utambulisho wetu wa kweli—si kushindwa kwetu,si hali zetu, bali nafasi yetu kama watoto wapendwa wa Mungu.

## Tafakari:

Kujua kwamba ulichaguliwa "kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu" kunabadilisha vipi mtazamo wako kuhusu changamoto unazopitia sasa au hisia za kutotosha?

## Ombi:

Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru kwa baraka zako juu ya maisha yetu. Tunaomba Roho Mtakatifu azidi kutukumbusha sisi ni nani ndani ya Kristo Yesu.



# Siku ya 9: Nyumba ya Neema

## Waefeso 2:19–22

*Kwa hiyo, ninyi si wageni tena wala wahamiaji, bali ni wananchi pamoja na watakatifu na watu wa nyumbani mwa Mungu... Ndani yake ninyi pia mnajengwa pamoja ili kuwa makao ambayo Mungu anaishi ndani yake kwa Roho wake.*

### Ibada:

Sisi si watu wa nje tena, bali ni sehemu ya nyumba ya Mungu. Sio wageni tu katika nyumba ya Mungu, bali ni familia. Neema ya Mungu haitukaribishi tu; inatujenga upya. Familia na nyumba zetu zinaweza kuwa "nyumba ya neema," sehemu ambayo Mungu anaweka makao yake. "Nyumba ya neema" haifafanuliwi na usanifu au mapokeo, bali na hisia ya kuwa sehemu ya familia. Ni mahali ambapo kila mtu anapendwa na kuthaminiwa, mahali tunapoombana na kutumikiana kwa upendo. Hii haiondoi migogoro au kutokuelewana, bali inamaanisha kwamba tunayaishi matunda ya Roho kati yetu. Kadiri tunavyozidi kuombana, ndivyo tunavyokuwa wavumilivu zaidi, watu wa neema zaidi, na tusamehevyo zaidi. Kila hatua ya ukuaji wa kiroho ndani ya familia ni kama kuweka tofali katika ujenzi wa nyumba ya Mungu. Tunapoombana na kuomba pamoja, tunasimama katika nafasi ya kusaidiana na kubeba mizigo ya kila mmoja, wakiwemo wale wa familia zetu ambao bado hawamjui Kristo. Hii pia hutupa nafasi ya kuwaombea ili nao wawe sehemu ya nyumba ya Mungu.

### Tafakari:

Huenda wewe ndiye Mkristo pekee katika familia yako, au pengine kuna wengi wenu wanaomkiri Yesu kama Bwana. Ni katika njia zipi tunaweza kueneza neema ya Mungu kwa wanachama wa familia zetu?

### Ombi:

Bwana, sisi ni sehemu ya nyumba yako. Tusaidie kufanya familia zetu kuwa mahali ambapo neema yako inahisiwa na Roho wako anakaribishwa. Maisha yetu na jinsi tunavyotendeana yaakisi moyo wako; tumewe kutumikiana kwa upendo na kuwa wapole na wenye neema kwa kila mmoja. Tuwe ushuhuda kwa majirani kwamba Mungu anaishi hapa, na wale wasiokujua wakuje kukujua kwa sababu sisi ni nyumba yako. Amina.



# Siku ya 10: Maombi ya wanandoa na mahusiano

**Waefeso 5:21**

*Nyenyekeaneni ninyi kwa ninyi kutokana na kumcha Kristo.*

**Ibada:**
Ndoa ni agano linalopaswa kuonyesha upendo wa Kristo kwa Kanisa. Katika Waefeso 5:21–33, Paulo anaonyesha picha ya kunyenyekeana, upendo wa kujitoa, na umoja wa kiroho. Aya hii inawataka mume na mke wote wawili kumwiga Kristo; mume kwa kupenda kwa kujitoa bila ubinafsi, na mke kwa kujibu kwa heshima na kuamini. Wawili wanakuwa mmoja, wakionyesha ukaribu uliopo kati ya Kristo na Bibi Arusi wake.

Wakati maombi yanakuwa kama mpigo wa moyo, ndoa hustawi. Upendo ambao Paulo anaelezea hauendelezwi na hisia pekee; unakuzwa kupitia maombi. Kumwombea mwenzako wa ndoa ni mojawapo ya njia zenye nguvu zaidi za kumpenda. Hapa ndipo Mungu hubadilisha mioyo.

**Tafakari:**
- Je, maneno na matendo yetu kwa kila mmoja yanaonyesha upendo na neema ya Kristo?
- Je, tunaomba si tu kwa ajili ya mwenzi wetu, bali pia pamoja na mwenzi wetu?

**Maombi ya Wanandoa:**
Bwana, tufundishe kuwaombea wengine kwa huruma na kwa kudumu. Tusaidie kuonana kwa jinsi unavyotuona. Maombi yetu yawe chanzo cha uponyaji, nguvu na furaha. Tuunganishe katika kusudi, ulinde upendo wetu, na uongeze imani yetu. Ndoa yetu iakisi utukufu wako. Amina.



# Siku ya 11: Maombi ya wazazi na watoto (mahusiano)

**Waefeso 6:1-4**

*Akina baba, msiwachokoze watoto wenu; bali waleeni katika malezi na maonyo ya Bwana.*

## Ibada:

Neno la Kiyunani lililotumika hapa hutafsiriwa mara nyingi kama "akina baba," lakini kwa ujumla linamaanisha "wazazi." Kuombea na kuomba pamoja na watoto ni jukumu la pamoja kwa wazazi wote wawili. Kuombea watoto ni rahisi, lakini kuomba pamoja nao wakati mwingine ni changamoto. Ni rahisi kumkaripia mtoto kisha kwenda mahali pako pa maombi kumwombea. Hata hivyo, ni vigumu zaidi kumkasirisha mtoto kisha kupiga magoti pamoja naye katika maombi.

Paulo anashauri wazazi kutoanza kwa kuwachokoza au kuwakatisha tamaa watoto wao, ili iwe rahisi kuwafundisha na kuwaelekeza katika imani. Kuombea na kuomba pamoja na watoto wetu hakupaswi kupitwa na wakati. Hata wanapokua na kuwa watu wazima, kuomba pamoja nao bado ni njia muhimu ya kuwaongoza na kuwaelekeza katika Bwana.

## Tafakari:

- Je, ni rahisi zaidi kwako kuwaombea watoto/wazazi wako au kuomba pamoja nao?
- Unawezaje kutumia kanuni ulizojifunza katika siku 21 za maombi kuboresha maombi yako kwa ajili na pamoja na watoto/wazazi wako?

## Ombi:

Baba wa Mbinguni, tunakushukuru kwa kuwa mzazi mkamilifu kwetu. Tusaidie kuiga mtindo wako wa malezi katika maisha yetu na kuomba kwa ajili ya watoto wetu na/au wazazi wetu, na kuomba pamoja nao pia.
Kwa jina la Yesu. Amina.



# Siku ya 12: Wafanya Amani

**Waefeso 4:25–27**

*Mkikasirika, msitende dhambi; msikubali kukaa na hasira kutwa nzima  na kumpa shetani nafasi.*

**Ibada:**
Dunia ya leo inapigania maslahi yake binafsi usiku na mchana.
Hofu ya changamoto za kesho inawasukuma watu kushikilia mamlaka na kujitafutia uhuru wao na familia zao, hata kwa vizazi vijavyo. Mara nyingi hali hii husababisha udanganyifu, uongo, wizi, usaliti, vurugu, na kuwatumia wengine ili kuonekana wenye nguvu na wasioweza kupuuzwa.
Lakini ikiwa hii ndiyo nia ya mwanadamu, mapenzi ya Mungu ni nini katika mfumo kama huu?
Biblia inatufundisha kwamba, licha ya hofu na wasiwasi wetu, lazima tujitahidi kukuza maadili yanayodhihirisha na kuthibitisha tunda la mabadiliko yetu: ukweli katika mambo yote, nyakati zote. Ukweli lazima uwe msingi wa maisha yetu ya kila siku.
Palipo na ukweli, uongo hukimbia.
Palipo na ukweli, hasira na matokeo yake hupotea.
Palipo na ukweli, upendo wa Mungu na haki yake hutawala.
Mtume Paulo anawasilisha ukweli na kujidhibiti kama masharti muhimu kwa mageuzi yetu katika Kristo Bwana wetu.
Kwa hiyo, kila mmoja wetu ajitahidi kwa bidii kufuata ukweli na kujidhibiti, ili ushuhuda wa maisha yetu hapa duniani ulete sifa na utukufu kwa Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo.
Sisi tumeumbwa kwa sura ya Kristo, na ushuhuda wetu unaonyesha nguvu ya dhabihu yake.

**Ombi:**
Bwana, nakushukuru kwa upendo na neema yako maishani mwangu.
Ninakuja mbele zako kama mche dhaifu, nikiomba Uniongoe.
Ninatambua mapungufu na udhaifu ndani yangu vinavyonivuta mbali na Wewe.
Ninatamani kukupendeza—nisaidie na uniongoze.
Vunja ndani yangu kila hali isiyoendana na kusudi lako maishani mwangu.
Nakutegemea: niongoze na unifinyange niwe mtu unayemtaka niwe.
Nakupenda, Bwana, na natamani kukuheshimu.
Naweka tumaini langu ndani Yako—yaongoze hatua zangu, Bwana.
Asante kwa kunisikia na kwa kulifanya maisha yangu kuwa ushuhuda wa sifa na utukufu wa Jina Lako.
Amina.



# Siku ya 13: Mahusiano Kazini

**Waefeso 6:7**

*Toeni huduma yenu kwa moyo wote, kama vile mnamtumikia Bwana na sio watu.*

### Ibada:

Aya hizi za Biblia zinatusaidia kuelewa wajibu wa mfanyakazi Mkristo na wajibu wa bosi katika familia ya Kikristo. Zinatoa ufahamu wazi kwamba Mkristo anapaswa kuangalia kazi yake kama baraka kutoka kwa Bwana na kutenda kazi ili kumpendeza Bwana, si kumfurahisha bosi wake. Kwa namna hii, mfanyakazi Mkristo anapaswa kufanya kazi kwa kumcha Mungu, akiepuka mabaya, na kufanya kazi kwa bidii ili kuwa na tija kwa kutambua kwamba kazi yake ni sehemu ya ibada kwa Mungu.

Wajibu wa bosi ni kuwapenda wafanyakazi wao na kuwachukulia kama ndugu wa Kikristo walioumbwa kwa sura ya Mungu. Bosi Mkristo lazima aepuke kuwakatisha tamaa wafanyakazi wake na awatendee kwa wema kwa neema ya Mungu. Pia, mabosi Wakristo wanapaswa kuwalipa wafanyakazi wao kwa upendo na kwa haki.

### Tafakari:

- Ni kwa jinsi gani Wakristo wanaweza kuwatendea wafanyakazi wao kama ilivyopendekezwa katika Waefeso 6:5–9?
- Mfanyakazi Mkristo anawezaje kuonyesha imani yake kwa Mungu katika sehemu yake ya kazi?

### Ombi:

Bwana wa kazi na pumziko, nakushukuru kwa zawadi ya kazi na jamii yetu kazini. Ubariki wenzangu kwa nguvu, ubunifu na umoja. Tusaidie kuungana kwa wema, kuwasiliana kwa neema, na kufanya kazi kwa kusudi. Kazi yetu na iakisi ukamilifu wako, na mahusiano yetu yaakisi upendo wako. Amina.



# Siku ya 14: Vita vya Kiroho Katika Familia

**Waefeso 6:18**


*Ombeni wakati wote katika Roho, katika sala zote na maombi. Kwa hiyo muwe macho na siku zote endeleeni kuwaombea watu wote wa Mungu.*

**Ibada:**
Hakuna kitu adui wa Mungu angefurahia zaidi kuliko kuvunja ndoa na familia. Familia zenye utauwa na afya ni ishara zinazoelekeza wengine kwenye umoja wa Mungu Utatu. Tangu mwanzo wa familia, katika simulizi la Kaini na Habili, tumeona adui akijaribu (na kufanikiwa katika Mwanzo 4) kuharibu familia.

Lakini hii si sababu ya kuogopa. Kujua kuwa familia zetu ni shabaha kunapaswa kututia moyo "kuomba katika Roho kila wakati kwa kila aina ya maombi na sala." Maombi—hasa maombi tukitumia Neno la Mungu—ndiyo silaha zetu za kushambulia adui. Kupitia maombi yetu, Mungu anashinda mipango ya adui.

**Tafakari:**
Ni andiko gani unaweza kuliombea familia yako leo?

**Ombi:**
Baba wa Mbinguni, tunakushukuru kwa kutuumba tuishi katika jamii ya familia ili kuwaelekeza wengine Kwako. Uwalinde wanachama wote wa familia yangu leo dhidi ya yule mwovu. Kwa jina la Yesu, Amina.



# Siku ya 15: Kusudi la Mungu kwa kanisa

**Waefeso 3:10**

*Yeye alikusudia kwamba sasa, kwa njia ya kanisa, hekima yote ya Mungu ipate kufahamika kwa mamlaka na nguvu zote katika makao ya mbinguni.*

**Ibada:**
Kanisa halipo tu kwa ajili ya ushirika au mkusanyiko wa watakatifu. Aya hii inatuambia kwamba kusudi la Mungu kuhusu kanisa ni kwamba Yeye Mwenyewe ajulikane. Mkakati wa Mungu wa kufunua hekima yake si kupitia hotuba za kuvutia au ishara na miujiza, bali ni kupitia sisi—kanisa. Sio jengo, bali mwili hai wa waamini. Tunapomruhusu Mungu kutujenga, kutuunda, kututakasa hadi tunakuwa mwili mmoja wa Kristo bila kujali kabila, taifa au tamaduni, tunaonyesha hekima yake si duniani tu bali hata katika ulimwengu wa mbinguni. Kanisa halipo kwa ajili ya utukufu wake au jina lake, bali kwa ajili ya kumtambulisha Mungu kupitia Yesu Kristo. Tunapoomba, "mapenzi yako yatimizwe duniani kama yalivyo mbinguni," tunaomba Mungu ajifunue. Na anapojifunua, anayetukuzwa ni Yeye. Neno "manifold" linamaanisha utofauti wenye utajiri na uzuri kama urembo wa kushonwa unaojumuisha nyuzi nyingi tofauti. Vivyo hivyo, Mungu analijenga kanisa lake kwa kuwaleta watu kutoka makabila, mataifa, tamaduni na asili tofauti ili wawe kitu kimoja—kanisa, mwili wa Kristo ambamo Mungu mwenyewe anakaa.

**Tafakari:**
Fikiria njia ambazo kanisa lako, huduma yako, au uongozi wako unaweza kuonyesha hekima yenye sura nyingi ya Mungu

**Ombi:**
Bwana, sisi ni kanisa lako. Tunatamani kukuona ukitukuzwa ndani yetu na kupitia kwetu. Hatuko kila mara vile tunavyopaswa kuwa kama kanisa; wakati mwingine tunajishughulisha zaidi na kujinua sisi wenyewe. Tusaidie kutambua kwamba kusudi na utume wa kanisa ni kukufanya Wewe—Mungu Mwenyezi—ujulikane. Na kama kuna kitu tunachofanya au tulichokuwa ambacho hakipatani na kusudi lako, Roho Mtakatifu na atukumbushe. Utukuzwe ndani na kupitia kanisa lako. Amina.



# Siku ya 16: Umoja na Kristo

**Waefeso 2:11–17**

*Kwa hiyo, kumbukeni kwamba zamani ninyi mliokuwa Wamataifa kwa kuzaliwa na kuitwa "wasiotahiriwa" na wale wajitaho nao "waliotahiriwa" (kutahiriwa huko kukifanywa mwilini kwa mikono ya wanadamu)— kumbukeni kwamba wakati huo mlikuwa mbali na Kristo, mkiwa hamna uraia katika Israeli na wageni... Alikuja akahubiri amani kwenu ninyi mliokuwa mbali na amani kwa wale waliokuwa karibu.*

**Ibada:**
Maisha bila Kristo ni maisha yaliyopungukiwa kusudi la mwisho na tumaini la milele. Kristo Yesu ndiye "tumaini la utukufu." Tumaini hili linapita hali za duniani kwa sababu limeegemezwa kwenye tabia ya milele na kazi iliyokamilishwa ya Mwokozi wetu. Wakati dunia inatoa suluhisho za muda na starehe za kupita, upatanisho wa Kristo unatoa mabadiliko ya kudumu na furaha ya milele.

Ushirika kati ya mwanadamu na Kristo ni umoja wa ndani unaobadilisha kiini cha utu wetu. Kupitia kazi yake ya ukombozi iliyotimizwa msalabani, Kristo alivunja ukuta wa dhambi uliotutenganisha na Mungu na kututenganisha sisi kwa sisi, akitufungulia njia ya kurejeshwa kwa uhusiano wa kweli na mawasiliano ya dhati.

Kanisa barani Afrika limesimama mahali pa kipekee pa kuonyesha nguvu hii ya upatanisho ya Kristo, likiwa mashahidi wa madhara ya mgawanyiko na pia nguvu ya kubadilisha ya injili. Kupitia jumuiya ya Kikristo ya kweli inayovuka mipaka ya kikabila, kiuchumi, na kisiasa, kanisa linaweza kuwa taa ya tumaini kwa bara na ulimwengu.

**Tafakari:**
Ni kwa jinsi gani Kanisa linaweza kukuza na kuonyesha amani katikati ya vita, kukata tamaa, na hali zinazoonekana kutokuwa na tumaini?

**Ombi:**
Baba wa Mbinguni,
Tunakushukuru kwa zawadi kuu ya upatanisho kupitia Mwanao, Yesu Kristo. Kupitia damu yake ya thamani iliyomwagika msalabani, umetuletea umoja wa kina na Wewe na sisi kwa sisi kama wanachama wa mwili wake. Tunakusifu kwa sababu umoja wetu na Kristo haujategemea matendo yetu, mafanikio yetu, au mali zetu, bali unategemea neema yako na kazi iliyokamilishwa ya Yesu. Kwa jina la Yesu, Amina.



# Siku ya 17: Rasilimali Isiyo na kikomo

**Efésios 3:16-17a**

*Ninaomba kwamba kwa utajiri wake wa utukufu awatie nguvu kwa uwezo wa Roho wake katika utu wenu wa ndani, ili Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani.*

**Ibada:**
Ugonjwa wa akili unaongezeka duniani kote. Inaonekana kuathiri sana vijana, na baadhi ya wataalamu wanaiita kizazi cha Gen Z kuwa Kizazi Chenye Wasiwasi. Hili linapaswa kuwa jambo la kututia moyo sisi katika Ukanda wa Afrika wa Kanisa la Nazarene, kwa kuwa umri wa wastani wa bara la Afrika ni miaka 19, ambao upo ndani ya umri wa Gen Z. Lakini tunapata moyo kwa sababu tunajua kwamba "kwa utajiri wake wa utukufu, [Mungu] atatupa nguvu kwa uwezo wa Roho wake katika utu wetu wa ndani." Mungu, ambaye huangalia moyo, anajali utu wetu wa ndani na afya ya akili, si afya ya kiroho tu. Basi tujitoe katika kuwaombea watu wote wa Mungu, hasa vijana, kwa ajili ya ustawi wao wa akili. Nguvu ya Roho Mtakatifu ndiyo rasilimali isiyo na kikomo ya kuutia nguvu kanisa.

**Tafakari:**
Ni kijana gani au vijana gani unaweza kujitolea kuwaombea leo, hasa kwa ajili ya afya yao ya akili?

**Ombi:**
Baba wa Mbinguni, tunakushukuru kwa kujali utu mzima wa mwanadamu na kwamba utajiri wako wa utukufu hauishii katika mwili au roho tu. Asante Roho Mtakatifu kwa kuwa na nguvu za kuutia nguvu utu mzima. Tusaidie kuwa waaminifu katika kuwaombea wale wanaoathiriwa na ugonjwa wa akili. Kwa jina la Yesu. Amina.



# Siku ya 18: Kuandaliwa kwa ajili ya huduma

## Waefeso 4:11-13

*Naye ndiye aliyowapa wengine kuwa mitume, wengine manabii, wengine waijilisti, wengine wachungaji na walimu, ili kuwatayarisha watakatifu kwa kazi ya huduma, kwa kujenga mwili wa Kristo; hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumjua Mwana wa Mungu, tufikie kuwa watu waliokomaa, wenye kiwango cha ukamilifu wa Kristo.*

### Ibada:

Katika bara hili kubwa la Afrika na hata nje yake, Kristo mwenyewe ameweka kwa mpangilio zawadi zake ndani ya kanisa lake. Kama vile Paulo aliwaandikia Waefeso, Yesu amelipa kanisa mitume wanaoanzisha kazi mpya, manabii wanaozungumza moyo wa Mungu, waijilisti wanaowafikia wasiofikiwa, wachungaji wanaotunza kwa upole, na walimu wanaofungua Maandiko kwa uwazi.

Ni muhimu kuelewa kwamba zawadi hizi hazijatolewa kwa ajili ya utukufu binafsi au kujenga matabaka ya kiroho. Zimetolewa "ili kuwatayarisha watakatifu kwa kazi ya huduma." Kila muumini, awe katika kanisa kubwa la maelfu au katika kanisa la nyumbani chini ya mti wa mbuyu, ameitwa katika huduma. Vipawa hivi vitano vipo ili kufundisha, kutia moyo, na kuwaachilia waumini wote katika kazi ya huduma.

Lengo ni la kina: umoja wa imani, ukomavu katika Kristo, na kukua hadi kufikia utimilifu wake. Kama waamini, tumeandaliwa kwa makusudi ili kuhudumu. Hii ndiyo maono ya Kristo kwa kanisa lake barani Afrika na duniani—si mashindano kati ya madhehebu au makanisa yaliyotengwa kwa sababu ya vipawa vyetu, bali kuwa mwili mmoja ulio na umoja, uliokomaa na kamili, unaodhihirisha utukufu wake kote barani.

### Tafakari:

Mungu anakuita utumie vipawa vyako vipi ili kulijenga na kuliimarisha kanisa lako la nyumbani?

### Ombi:

Mungu wetu na Baba yetu, tunakushukuru kwa zawadi ulizolipa kanisa lako. Umetuita na kutuaminisha vipawa vikuu kwa kusudi moja la kuwatia nguvu na kuwatayarisha watu wako. Tusaidie kutumia vipawa vyetu kwa hekima, si kwa faida binafsi bali kwa ajili ya utukufu wako. Tunaomba Roho wako atusaidie kukua katika umoja wa imani na ukomavu katika Kristo. Kwa jina la Yesu, Amina



# Siku ya 19: Kukua pamoja katika upendo

**Waefeso 4:10-18**

*Kutoka kwake mwili wote, unaounganishwa na kushikiliwa pamoja na viungo vyote vinavyounga mkono, hukua na kujijengea katika upendo, kadri kila sehemu inavyofanya kazi yake.*

**Ibada:**
Kupaa kwa Kristo mbinguni kuleta vipawa tofauti ndani ya kanisa: baadhi ya waijilisti, wachungaji, na walimu, ambavyo hutolewa kututayarisha kwa kazi ya Mungu na kujenga mwili wa Kristo, ili tufikie umoja na ukomavu katika imani. Hii ni ili tusizungushwe na mafundisho ya uongo, bali tuweze kusema kweli kwa upendo na kuishi kwa njia tofauti. Lakini vipawa hivi si vya kuinua mtu binafsi, bali ni vya kuijenga mwili wa Kristo.

Tunakua vyema zaidi tunapokua pamoja. Ukimavu wa kiroho si safari ya mtu mmoja. Ni wito wa pamoja kuwa "waliokomaa, wenye kufikia kiwango kamili cha ukamilifu wa Kristo" (v.13). Hii inamaanisha kujifunza kusema kweli kwa upendo, kuhimili upepo wa mafundisho ya uongo, na kujikita katika Kristo, Kichwa chetu. Hii ni maono ya umoja, si usawa wa kila mmoja. Kila sehemu ni muhimu. Kila kipawa kinachangia. Kila sauti inatia nguvu. Iwe unafundisha vijana, kuombea, au kuhubiri, kazi yako ni sehemu ya mchoro wa kimungu uliochongwa kwa upendo.

**Tafakari:**
- Ninawezaje kujenga wengine kwa upendo?
- Nina sehemu gani ninayoichangia katika ukomavu wa mwili?

**Ombi:**
Baba, tunakushukuru kwa zawadi ya Roho Mtakatifu na vipawa mbalimbali ulivyopewa kanisa. Tunaomba utusaidie kutumia vipawa vyetu kuhudumia wengine. Tuelekeze kusema kweli kwa upendo na kuishi tofauti na mifumo ya dunia. Amina.



# Siku ya 20: Kito cha Mungu

**Waefeso 2:8-10**

*Kwa maana ni Kwa neema umeokolewa kupitia Imani. Na hii sio kutoka kwako, ni zawadi ya Mungu. Sio Kwa kazi ila hakuna mtu anayeweza kujivunua. Kwa kuwa sisi ni kazi ya mikono ya Mungu, kuumbwa katika Kristo Yesu ili tutende mema ambayo Mungu alituandalia awali.*

**Ibada:**

Hiki kifungu cha biblia inatusaidia kuelewa Bora mambo yafuatayo:

- Wokovu ni zawadi ya Mungu ambayo haitegemei nguvu na kazi ya binadamu. Wokovu wa binadamu ni matokeo ya upendo wa Mungu unao onyeshwa kupitia maisha ya Yesu Kristo ambaye alikubali kifo Kwa ajili yetu (5:8). Tunahitaji Imani ili tufurahie wokovu wa Mungu na upendo ambayo Mungu alituonyesha kupitia upatanisho wa damu  ya Yesu Kristo uliomwagika msalabani.
- Wakristo ni Kito cha Mungu walioumbwa na kusudi ya kumtukuza Mungu katika maisha Yao ya Kila siku.
- Kama Kito cha Mungu, tumeumbwa ili tuabudu Mungu, tumfurahishe Kwa kuishi maisha ya utakatifu ambayo ni mipango ya Mungu kwetu.

**Tafakari:**

- Je, twaweza pataje wokovu wa Mungu?
- Ni nini maana (mbinu) za wokovu wa Mungu Kwa maisha ya binadamu?

**Ombi:**

Mungu muumbaji wetu, Asante Kwa kutuunda Kwa kusudi na upendo wako. Sisi ni Kito chako, uliotengenezwa Kwa neema, kuitwa Kwa kazi nzuri na kuumbwa Kwa maonyesho ya ukuu wako. Tusaidie tutembee kikamilifu na kuhudumia ulimwengu na ujasiri, tukikuheshimu katika Kila hatua tunayopiga. Amina



# Siku ya 21: Vita vya kiroho kanisani

## Waefeso 6:10-12

*Mwishowe, uwe na nguvu katika Bwana na Kwa nguvu yake kuu,  vaa silaha kamili ya Mungu ili muweze kuchukua msimamo dhidi ya mpango ya shetani.*

Maandiko yakumbusha waumini kuwa maisha ya Ukristo Yana Vita vya kiroho hatuwezi pigana na nguvu zetu. Ushindi yaja kupitia nguvu za Mungu tunaopata kupitia Imani, maombi na utiifu.


Mwishowe, Paulo anatamatisha barua yake na kumbusho lenye maana. Baada ya mafundisho yake kuhusu umoja na upendo na kuishi kama watoto wa nuru, anageuka Kwa ukweli wa Vita vya kiroho. Kuwa na nguvu Kwa Mungu . Nguvu yetu hayatoki kwetu Bali Kwa uhusiano na Mungu. Ni wito wa kumtegemea kabisa na nguvu zake kuu. Hiyo nguvu ndiye nguvu iliyo fufua Yesu kutoka Kwa wafu.

### Ombi:

Mungu wa mbinguni tunakuja mbele zako leo kama watoto  wako na kanisa lako. Bwana tunajua ya kwamba adui anatafuta  kuiba, kuua, kuharibu lakini wewe umekuja ili tuwe na uzima tele.

Katika jina kuu la Yesu, tunachukua mamlaka juu ya Kila roho ya utengano, kuchanganyikiwa, masengenyo, ugomvi yanayotafuta kuingia kanisani. Tunafunga Kila mipango ya adui itakayojaribu kuleta utengano, usumbufu na kukatisha tamaa kati ya watoto wako.

Mungu funika Kila mchungaji, kiongozi na mshirika chini ya damu ya thamani ya Yesu. Linda mioyo yetu, akili zetu kutokana na uongo na uoga na udanganyifu. Zingira kanisa lako na malaika wako kama ua wa ulinzi. Tunakiri kwamba hakuna silaha iliyoundwa kinyume na kanisa itakayonawiri na Kila ulimi itakayoinuka kinyume yake siku ya hukumu italaaniwa. Roho mtakatifu jaza mahali hapa na uwepo wako, leta ufufuo na uupya katika jina kuu ya Yesu. Tunatangaza ushindi juu ya Kila uvamio na uongo na Kila msingi katika jina la Yesu. Amina.


Asante
Kanisa la Mnazareti - Afrika